

AFRIPRISE
INVESTMENT PLC.

TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 21 WA MWAKA

2026

TAARIFA ZA JUMLA

USAJILI WA OFISI

Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE

(Imesajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)
Namba ya Usajili: 38280
Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN) 103-410-444

Nchi ya Usajili na Makao ya Kampuni:	Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Aina ya Shughuli za Kampuni:	Investment in stocks, shares and bonds
Wakurugenzi:	Fortunatus Makore Magambo Prof. Lucian A. Msambichaka Joseph Matanga Kahungwa Magdalene N. E. Mkocha Nathan E. Mnyawami Adv. Valentino D. Maganga CPA. Vicent B. Minja
Anuani ya Ofisi:	24th Floor PSSSF Millennium Tower II, Bagamoyo road, Kijitonyama, Dar es Salaam.
Anuani:	P. O. Box 72678 Dar es Salaam Tanzania
Banki:	CRDB Bank Plc P.O. Box 2302 Dar es Salaam
Auditors:	Auditax International Certified Public Accountants in Public Practice Dar es Salaam
Katibu:	Peter William Kifunguomali

TAARIFA YA KUITISHA


MKUTANO NA AKIDI

Wanahisa wanaombwa kuzingatia taarifa iliyotolewa kulingana na kifungu Namba 33 cha Kanuni za Kampuni kinachohusu uitishaji wa Mkutano Mkuu wa Wanahisa.

Wanahisa wanaombwa kuzingatia kuwa, akidi kwa mujibu wa kifungu Na. 38 cha Kanuni za Kampuni ni idadi ya wanahisa wasio-pungua 10 wanaomiliki hisa zaidi ya asilimia 50.

KUPOKEA AJENDA

Wanahisa mnaombwa kupokea Ajenda kama zilivyowasilishwa.



TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA MOJA WA WANAHISA WA KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA AFRIPRISE

Kampuni inapenda kuwajulisha Wanahisa wote kuwa Mkutano Mkuu wa Ishirini na Moja wa Wanahisa wa Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE utafanyika siku ya Jumamosi, 21/11/2026, kuanzia saa 3:00 Ahsubuhi, kwa njia ya mtandao. Wanahisa wote watapokea maelekezo ya kujiunga na kushiriki Mkutano kupitia ujumbe wa simu au barua pepe, pamoja na kiungo cha Mkutano.

DONDOO ZA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA MOJA (KWA AJILI YA MWAKA WA FEDHA 2025):

1. Kufungua rasmi Mkutano Mkuu wa Ishirini na Moja
2. Kupokea na kuridhia Dondoo za Mkutano Mkuu
3. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Ishirini
4. Kujadili Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Ishirini
5. Kupokea, kujadili na kuridhia:
   a. Taarifa ya Mwenyekiti wa Bodi
   b. Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji
   c. Taarifa ya Wakurugenzi Pamoja na Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2025
6. Kupokea, Kujadili na kuridhia Pendekezo la Gawio kwa mwaka wa fedha 2025
7. Kupokea, kujadili na kuridhia Pendekezo la uteuzi wa Mkaguzi wa Mahesabu kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Desemba, 2026
8. Kupokea, kujadili na kuridhia Pendekezo la Malipo ya Wajumbe wa Bodi kwa mwaka, 2026
9. Kupokea na Kujadili mapendekezo rasmi yaliyowasilishwa na Wanahisa
10. Kufunga Mkutano

KUFUNGA MKUTANO MKUU

Maelezo Muhimu kwa Wanahisa:

1. **Mapendekezo toka kwa Wanahisa:** Wanahisa wanahimizwa kuwasilisha mapendekezo yao kwa maandishi kwa Katibu wa Kampuni kabla ya tarehe 13 /11/2026 ili yaweze kujumuishwa katika Dondoo namba 10 ya Mkutano.
2. **Taarifa ya Mwaka na Makabrasha:** Taarifa ya Mwaka 2025 pamoja na Makabrasha ya Mkutano yatapatikana kwenye tovuti ya Kampuni kuanzia 13 /11/2026 kupitia anwani: ***https://www.afriprise.co.tz***
3. **Uwakilishi:** Kama Mwanahisa hataweza kuhudhuria Mkutano, anaombwa kuteua mwakilishi kwa kujaza Fomu ya Uwakilishi inayopatikana kwenye tovuti ya Kampuni www.afriprise.co.tz. Fomu zilizojazwa zitumwe kwa Katibu kupitia barua pepe: ***info@afriprise.co.tz*** au kwa WhatsApp namba: ***0757 138 048***, kabla ya 2026, saa 10:00 jioni.

Imetolewa kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi

Peter W. Kifunguomali
Katibu wa Kampuni
Tarehe: **21 Novemba 2026**

KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI WA WANAHISA ULIOFANYIKA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 15 NOVEMBA, 2025 KWA NJIA YA MTANDAO.

20.1 WALIOHUDHURIA

- Bw. Fortunatus Magambo – **Mwenyekiti**
- Bw. Peter W. Kifunguomali – **Katibu**

Kumbuka: Orodha kamili ya Wajumbe wa Bodi, Menejimenti, Wanahisa, na Wawakilishi waliohudhuria mkutano huu kwa njia ya mtandao imeambatanishwa kwenye kumbukumbu hizi kama Kiambatisho Namba 1.

20.2 UFUNGUZI WA MKUTANO

Mwenyekiti alifungua mkutano rasmi saa 3:19 Asubuhi baada ya kuthibitishiwa kuwa akidi imetimia kulingana na Kifungu Namba 38 cha Kanuni za Kampuni. Aliwakaribisha Wanahisa, Wajumbe wa Bodi, Wafanyakazi, na Wageni Waalikwa. Katika hotuba yake, alieleza mwelekeo wa kimkakati wa Kampuni na kupongeza mafanikio yaliyopatikana.

20.3 KUPOKEA NA KURIDHIA DONDOO ZA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI (20)

Katibu wa Bodi aliwasilisha dondoo na muundo wa ajenda za Mkutano Mkuu wa Ishirini (20). Baada ya mapitio, hakukuwa na mabadiliko au nyongeza yoyote, na wajumbe walizipitisha dondoo hizo kama zilivyowasilishwa kwa ajili ya kuongoza mkutano wa siku hiyo.

20.4 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI (20)

Katibu wa Bodi alisoma Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Ishirini (20) uliofanyika tarehe 23 Novemba 2024. Wajumbe walizipitia na kuthibitisha kuwa ni kumbukumbu sahihi za yaliyojiri, ambapo zilikubaliwa bila marekebisho na kusainiwa rasmi na Mwenyekiti pamoja na Katibu.

20.5 KUJADILI YATOKANAYO NA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA MKUTANO MKUU WA 20

Wanahisa walipokea na kuridhia ripoti ya utekelezaji wa maazimio yaliyopita kama ifuatavyo:

- **Gawio la 2023:** Kiasi cha TZS 13 kwa kila hisa kililipwa kikamilifu kwa wanahisa kuanzia tarehe 25 Novemba 2024.
- **Ukaguzi wa Hesabu:** Kampuni ya CROWE Tanzania ilikamilisha kwa ufanisi ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2024.
- **Idadi ya Wajumbe wa Bodi:** Azimio la kupunguza wajumbe wa Bodi kutoka saba (7)

hadi watano (5) kuanza kutekelezwa rasmi baada ya Bodi iliyochaguliwa mwaka 2024 kumaliza muda wake wa sasa.

20.6 KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA TAARIFA YA WAKURUGENZI KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA DESEMBA 2024

1. **Taarifa ya Mwenyekiti wa Bodi**: Alibainisha kuwa mwaka 2024 ulikuwa wa mageuzi makubwa kufuatia mchakato wa kubadili chapa (rebranding) na mkakati wa kupanua uwekezaji kikanda (EAC na SADC).
2. **Taarifa ya Afisa Mtendaji Mkuu (CEO)**: Bw. Peter Kifunguomali alieleza kuwa Kampuni ilipata mafanikio makubwa ya kifedha ambapo mapato ya uendeshaji yalikua kwa 36.7% (kufikia TZS bilioni 4.21), na faida halisi baada ya kodi iliongezeka kwa 72.3% (kufikia TZS bilioni 3.40). Thamani ya mali halisi ilifikia TZS bilioni 52.

Maoni na Majadiliano kutoka kwa Wanahisa:

- Walipongeza Bodi na Menejimenti kwa kupata matokeo mazuri ya kifedha na taarifa thabiti.
- Walishauri Bodi kuendelea kubuni mbinu za kuongeza mapato huku ikidhibiti kwa ukaribu matumizi ili kuepuka gharama zisizo za lazima.
- Walishauri Kampuni kuangalia fursa mpya za uwekezaji katika sekta ya viwanda.
- Taarifa ya Mwaka ya Wakurugenzi na Bodi inapitishwa kama ilivyowasilishwa.
- Wajumbe walipokea taarifa ya mahesabu ambapo Mkaguzi wa Nje alijulisha Mkutano kuwa Kampuni imepata **Hati Safi (Unqualified Audit Opinion)** kwa mwaka wa fedha wa 2024. Taarifa ilionyesha muundo wa uwekezaji kuwa imara (Hati Fungani 32%, Hisa 63%), na shughuli za Kampuni ziko salama kuendelea bila athari yoyote (going concern).

20.7 PENDEKEZO LA BODI KUHUSU MALIPO YA GAWIO KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA 31 DESEMBA, 2024

Bodi ilipendekeza kutoa gawio la TZS 18 kwa kila hisa (ongezeko kutoka TZS 13 ya mwaka wa 2023), na malipo yafanyike ndani ya siku tisini (90). Mkutano Mkuu uliridhia kwa kauli moja gawio la TZS 18 kwa kila hisa kama ilivyopendekezwa na Bodi.

20.8 UTEUZI WA MKAGUZI WA MAHESABU YA KAMPUNI KWA MWAKA WA FEDHA ILIOISHIA DESEMBA 31, 2025

Wajumbe walifahamishwa kuwa kampuni ya CROWE Tanzania ilihudumu kwa miaka saba (7) mfululizo na hivyo imefikia ukomo wa kisheria na maadili ya utawala bora, hivyo hawatateuliwa tena.
Mkutano Mkuu uliarifiwa, baada ya mchakato wa tathmini na mapendekezo kutoka Kamati ya Ukaguzi ya Bodi, kampuni ya Auditax International ilipendekezwa kutokana na

uzoefu wake mkubwa na sifa stahiki kwenye soko la hisa.
Mkutano Mkuu umeidhinisha kuteuliwa kwa Auditax International kuwa Wakaguzi wapya wa mahesabu ya Kampuni kwa mwaka wa fedha unaoishia Desemba 31, 2025, kwa ada ya TZS 22,000,000/= (Milioni Ishirini na Mbili) kabla ya kodi.

20.9 PENDEKEZO KUHUSU MALIPO YA WAKURUGENZI (DIRECTORS' FEES)

Kulingana na matokeo mazuri ya kifedha ya mwaka 2024, Menejimenti ilipendekeza malipo ya Wakurugenzi yasibadilike yabaki katika kiwango cha sasa. Iliazimiwa kuwa malipo ya Wakurugenzi wa Bodi (Directors' fees) kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba 2024 yawe kiasi cha TZS 6,200,000/= (Shilingi Milioni Sita na Laki Mbili) kwa kila Mjumbe wa Bodi.

20.10 UTOAJI WA HISA ZA UPENDELEO ZISIZO NA HAKI YA KUPIGA KURA ZENYE UWEZO WA KUKOMBOLEWA (NON-VOTING REDEEMABLE CUMULATIVE PREFERENCE SHARES)

Mkutano Mkuu ulijulishwa kuwa Bodi ilipitisha azimio la kutoa Hisa za Upendeleo kupitia mpango wa Private Placement ili kukusanya mtaji wa jumla ya TZS Bilioni 20 kwa ajili ya miradi ya kimkakati.

- **Mwekezaji Anayelengwa:** Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).
- **Mshauri wa Kisheria:** Endoxa Law.
- **Matumizi ya Mtaji:** Kuanzisha bidhaa mpya ya Unsponsored Depository Receipts kwenye soko la DSE, kuwekeza kwenye sekta ya viwanda kwa dhamana ya BoT, na kutoa mikopo kwa taasisi ndogo za fedha zilizosajiliwa.
- **Uamuzi:** Mkutano Mkuu uliridhia mpango huo na kuipa Bodi mamlaka kamili ya kuwasilisha maombi rasmi kwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) na kuandaa mikataba yote muhimu.

20.11 AJENDA YA 11: KUFUNGA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI

Mwenyekiti wa Bodi aliwashukuru wanahisa wote, Wajumbe wa Bodi, Menejimenti, na Wageni Waalikwa kwa ushiriki wao madhubuti na michango yao mizuri yenye lengo la kukuza Kampuni.
Mkutano ulifungwa rasmi saa 4:26 Asubuhi.

KUPOKEA NA KURIDHIA DONDOO ZA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA MOJA (21)

WASILISHO

Wanahisa wanaombwa kupokea na kuthibitisha Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa 20 uliofanyika tarehe 15, Novemba, 2025 kama kumbukumbu sahihi:-


> *"Azimio la 1/2025*
>
> *Imeazimiwa kuwa muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Ishirini uliofanyika tarehe 15/11/2025 ni kumbukumbu sahihi."*

YATOKANAYO NA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU ULIOPITA

KUMB	MAELEZO MAFUPI	AZIMIO LILILOPITISHWA	HALI YA UTEKELEZAJI
20/6/2025	**Malipo ya Gawio la Mwaka 2024:**	Kulipa gawio la TZS 18 kwa kila hisa (Jumla ya TZS 2,626,475,760/=).	**Imetekelezwa:** Malipo yalifanyika mara moja baada ya Mkutano. Wanahisa wenye Akauti za benki, na wengine kupitia mitandao ya simu.
20/7/2025	**Uteuzi wa Mkaguzi Mpya wa Nje:**	Kusitisha huduma za CROWE Tanzania baada ya ukomo wa miaka 7 na kumwajiri rasmi mkaguzi mpya.	**Imetekelezwa:** Kampuni ya Auditax International iliteuliwa rasmi kwa mwaka wa fedha 2025 kwa ada ya TZS 22,000,000/= (kabla ya kodi). Tayari walishapewa Mkataba
20/8/2025	**Malipo ya Wajumbe wa Bodi:**	Kulipa ada ya Wakurugenzi (Directors' fees) kwa mwaka wa fedha 2024.	**Imetekelezwa:** Kila mjumbe wa Bodi alilipwa kiasi cha TZS 6,200,000/= kama ilivyoidhinishwa na Mkutano Mkuu
20/9/2025	**Utoaji wa Hisa za Upendeleo (Preference Shares):**	Mchakato wa kutoa Non-Voting Redeemable Cumulative Preference Shares za hadi TZS bilioni 20 kupitia Private Placement.	**Imetekelezwa:** Bodi iliwasilisha maombi rasmi CMSA, kushirikiana na PSSSF kama mwekezaji mkuu, na kufanya kazi na Endoxa Law (Mshauri wa Kisheria) kuandaa nyaraka zote.

Jedwali na. 1

KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA TAARIFA YA WAKURUGENZI WA BODI YA KAMPUNI NA TAARIFA YA MAHESABU YALIYOKAGULIWA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2025.



Taarifa ya Mahesabu yaliyokaguliwa iko katika Taarifa ya Mwaka.



Taarifa ya Mwenyekiti wa Bodi

Ndugu Wanahisa,

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, ninayo heshima kubwa kuwasilisha **Taarifa ya Mahesabu ya Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE kwa mwaka 2025**

Mwaka huu umeashiria kipindi muhimu cha mpito katika historia ya Kampuni yetu, ambapo tulihitimisha mzunguko wa Mpango Mkakati wa miaka mitatu (2023 - 2025).

Utendaji wa kihistoria na kuongezeka kwa thamani ya kampuni Sokoni

Mwaka wa fedha 2025 umedhihirisha uthabiti, uwezo wa kukabiliana na changamoto, pamoja na uwazi wa mwelekeo wa kimkakati wa Kampuni yetu. Kufuatia mafanikio ya kurejesha ukuaji wa biashara mwaka 2024, kasi yetu ya maendeleo imeendelea kuimarika.

Ninayo furaha kuwataarifu kuwa thamani ya Kampuni yetu katika Soko la Hisa imeongezeka kwa kiwango kikubwa. Kutoka kiwango cha chini cha **TZS 150 kwa kila hisa mwezi Desemba 2022**, bei ya hisa iliongezeka hadi kufikia **TZS 495 kwa kila hisa mwezi Desemba 2025**, ikiwa ni ongezeko la takribani **asilimia 230**.

Kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2021, hisa za Kampuni zimeendelea kuuzwa kwa bei iliyo juu ya **Thamani Halisi ya Mali za kampuni kwa Kila Hisa (Net Asset Value – NAV)**, jambo linaloashiria imani kubwa ya wawekezaji na soko kwa ujumla kuhusu utendaji wetu bora wa kifedha na matarajio ya ukuaji endelevu.

Kuimarisha thamani kwa wanahisa

Ikiwa ni sehemu ya dhamira yetu ya kuendelea kuwaletea wanahisa wetu manufaa endelevu, Bodi ya Wakurugenzi imependekeza kutoa **gawio la TZS 23 kwa kila hisa**, lenye jumla ya **TZS 3,356,052,360.**

Pendekezo hili linaonyesha ongezeko kubwa ikilinganishwa na **gawio la TZS 18 kwa kila hisa** lililotolewa kwa mwaka uliopita, na linaakisi matokeo mazuri ya kifedha pamoja na msimamo imara wa Kampuni.

Matarajio ya mpango mkakati wa mwaka 2026 - 2028

Mwaka 2025, Bodi ya Wakurugenzi iliidhinisha **Mpango Mkakati wa Miaka 2026–2028**, ambao umeandaliwa ili kupanua wigo wa shughuli za Kampuni, kuimarisha uwepo wetu katika masoko mbalimbali, na Kuiwezesha Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE kuwa taasisi ya kifedha ya kikanda yenye ushindani mkubwa, ubunifu na ukuaji endelevu zaidi ya mipaka ya Tanzania kuelekea

katika masoko ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Kiini cha mkakati huu ni muundo wetu ulioboreshwa wa mtaji, unaojumuisha kuidhinishwa kwa Hisa za Upendeleo za Daraja A (Series A Non-Voting Redeemable Cumulative Preference Shares). Chombo hiki cha kifedha kitatuwezesha kupata mtaji wa muda mrefu usiopunguza umiliki wa wanahisa waliopo (non-dilutive funding), ili kutekeleza fursa za kimkakati zenye tija kubwa katika sekta za uchakataji wa mazao ya kilimo, usafirishaji na ugavi (logistics), pamoja na huduma za viwanda.

Dhamira yetu kwa uendelevu na utawala bora

Ukuaji wetu haupimwi kwa viashiria vya kifedha pekee. Tumebadilika kutoka katika mkakati wa kujihami dhidi ya hatari na kuelekea katika mkakati wa maendeleo unaoongozwa na misingi ya **Mazingira, Jamii na Utawala Bora (Environmental, Social and Governance – ESG).**

Mwaka 2025, tulijivunia kushiriki katika kampeni ya kitaifa ya upandaji miti, sambamba na kufanikisha matumizi ya mfumo wa utoaji taarifa usiotumia karatasi (paperless reporting) kupitia mageuzi ya kidijitali. Aidha, tunaendelea kuwa mfano wa kuigwa katika utawala shirikishi kwa kudumisha uwiano wa kijinsia wa asilimia 50 katika nguvu kazi yetu, pamoja na kuhakikisha wanawake wanawakilishwa kwa kiwango kikubwa ndani ya Bodi ya Wakurugenzi.

Uimara wa uendeshaji wa kampuni

Kwa kudumisha kiwango madhubuti cha ukwasi kinacholenga kuwa na fedha taslimu za kuendesha shughuli kwa angalau siku **120**, pamoja na kuondoa kabisa utegemezi wa mikopo ya benki, tumeihakikishia **Kampuni ya Uwekezaji ya Afriprise** uwezo mkubwa wa kukabiliana na mabadiliko na misukosuko ya soko.

Aidha, msisitizo wetu katika kuongeza ubora wa shughuli za uendeshaji kupitia mifumo ya kidijitali na uendeshaji wa kiotomatiki utaendelea kuimarisha uwezo wetu wa kubuni bidhaa changamani za kifedha na kusimamia hatari kwa usahihi na ufanisi wa hali ya juu.

Shukrani

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wakurugenzi wenzangu kwa maono yao ya kimkakati na ushauri wao muhimu. Pia ninawapongeza viongozi na timu yetu ya menejimenti kwa utekelezaji wao wenye nidhamu na kujituma katika kufanikisha malengo ya Kampuni.

Vilevile, ninawashukuru wanahisa wetu wote, hususan mwekezaji wetu mkuu, **Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (Public Service Social Security Fund – PSSSF)**, kwa imani yao na uungwaji mkono usioyumba waliouonyesha kwa Kampuni yetu.

Tunapoanza kutekeleza dira ya mwaka **2026 - 2028**, tunafanya hivyo tukiwa na msingi imara wa mtaji, utambulisho mpya wa kisasa wa chapa ya Afrika nzima (Pan-African Brand), na msimamo thabiti wa kutumia kikamilifu fursa zinazopatikana katika ukanda wetu.

Tunaendelea kujizatiti kuhakikisha kwamba Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE inabaki kuwa kichocheo muhimu cha mageuzi endelevu ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa manufaa ya wanahisa wetu, wadau wetu na jamii kwa ujumla.

Asanteni kwa kunisikiliza.



_____

Fortunatus Makore Magambo
Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi
Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE

Tarehe: 21 Novemba 2026



Taarifa ya Afisa Mtendaji Mkuu

Wadau Wapendwa,

Mwaka wa fedha 2025 umekuwa mwaka wa ukuaji uliokomaa na kuimarika kwa Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE. Tumefanikiwa kuvuka hatua ya kubadili utambulisho wa kampuni (rebranding) na kufanya maboresho ya kimfumo (restructuring), na sasa tumejijenga kuwa kampuni iliyoorodheshwa katika Soko la Hisa yenye faida, utendaji bora na msingi madhubuti wa shughuli za kiutendaji.

Muhtasari wa hali ya kifedha

Katika mwaka 2025, Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE imeonyesha uwezo wa hali ya juu wa kustahimili changamoto na kuendelea kukua. Thamani halisi ya mali za kampuni (Net Assets) ilifikia TZS bilioni 62.7, ikiwa ni ongezeko la asilimia 19 ikilinganishwa na mwaka uliopita. Matokeo haya yamezidi lengo la ukuaji la asilimia 5 Aidha, thamani ya kampuni katika Soko la Hisa imeongezeka kwa kiwango kikubwa, ambapo bei ya hisa ilipanda kutoka TZS 215 mwaka 2024 hadi kufikia TZS 495 kwa kila hisa mwezi Desemba 2025, jambo linaloonyesha kuongezeka kwa imani ya wawekezaji na soko kwa ujumla kuhusu utendaji na matarajio ya **ukuaji wa Kampuni.**

Jedwali Na. 1: *Viashiria vilivyowekwa vya Utendaji (Key Performance Indicators) lililowekwa katika Mpango wa Biashara wa Kampuni (Corporate Plan).*

Kiashiria	2025	2024
Thamani Halisi ya Mali (TZS '000) **(TZS '000)**	**62.70**	**52.5**
Faida Halisi Baada ya Kodi **(TZS '000)**	**4,520,821**	**3,395,505**
Mapato ya Kampuni **(TZS '000)**	**5,118,532**	**4,219,666**
Kiwango cha Faida kwa Uwekezajit (ROI)	**8%**	**7%**

Jedwali Na. 2: *Thamani ya Wanahisa na Taarifa za Soko la Hisa*

Kiashiria	2025	2024
Bei ya Hisa **(TZS)**	**495**	**215**
Faida kwa Kila Hisa **(TZS)**	**30.98**	**23.33**
Gawio Lililolipwa **(TZS '000)**	**3,356,052**	**2,626,476**

Mkakati wa uwekezaji na mgawanyo wa mali

Kwa mwaka wa fedha 2025, tuliendelea kuboresha muundo wa jalada letu la uwekezaji (portfolio) kwa kufanya uwiano mpya wa mali mbalimbali ili kuongeza uthabiti wa kifedha, kupunguza vihatarishi na kuboresha faida za muda mrefu.

Kutokana na mkakati huu, thamani ya uwekezaji katika hisa iliongezeka kwa kiwango kikubwa na kufikia TZS bilioni 44.6, hatua inayodhihirisha imani yetu katika fursa za ukuaji wa muda mrefu na uwezo wa jalada letu kuendelea kuzalisha thamani endelevu kwa wanahisa.

Jedwali Na. 3: *Mgawanyo wa Mali za Kampuni katika Uwekezaji (TZS '000)*

Aina ya Mali za Uwekezaji	2025	2024
Uwekezaji katika Hisa	**44,660,751**	**30,949,793**
Hatifungani za Serikali	**11,823,898**	**15,680,721**
Mali Nyingine za Kifedha	**3,297,672**	**2,355,000**

Mafanikio muhimu ya kiutendaji

- **Sekta ya Viwanda:** Tulianza mchakato wa ununuzi wa Mamba Ginger Growers Ltd, kampuni inayojishughulisha na uzalishaji wa bidhaa za tangawizi iliyoko Mkoa wa Kilimanjaro. Hatua hii inaashiria mwanzo wa utekelezaji wa mkakati wetu wa kuingia katika sekta ya uzalishaji wa viwandani na kuongeza wigo wa uwekezaji wa Kampuni.
- **Masoko ya Mitaji**: Tuliendelea kuimarisha uwepo wetu katika **Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) na Soko la Hisa la Nairobi (NSE)**, huku tukifanya maandalizi ya kuzindua **Mifuko ya Uwekezaji Inayouzwa Sokoni (Exchange Traded Funds – ETFs)**, ambayo itapanua fursa za uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na wa kikanda.

Matarajio ya baadaye: Kupanua wigo na kuongeza utaalam

Mpango Mkakati wa mwaka 2026 - 2028 umejengwa juu ya nguzo kuu tatu zifuatazo:


1. **Kuboresha Muundo wa Mtaji:** Kulenga kuelekeza kati ya asilimia 50 hadi 65% ya uwekezaji ufanyike kwenye hisa ili kuongeza ukuaji wa thamani ya muda mrefu.
2. **Upanuzi wa Kikanda:** Kutafuta na kutekeleza fursa za uunganishaji na ununuzi wa biashara (Mergers

and Acquisitions – M&A) ndani ya ukanda wa Afrika Mashariki ili kupanua shughuli za Kampuni na kuongeza ushindani wake.

3. **Ubunifu wa Bidhaa za Uwekezaji:** Kupanua upatikanaji wa huduma za uwekezaji kwa Watanzania kupitia uzinduzi wa Mifuko ya Uwekezaji Inayouzwa Sokoni (Exchange Traded Funds – ETFs), ili kuwezesha wananchi wengi zaidi kushiriki katika uwekezaji wa masoko ya mitaji kwa urahisi na kwa gharama nafuu.

Ninajivunia kwa dhati juhudi, weledi na kujituma kwa timu yetu, ambayo imeendelea kuifanya Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE kufikia mafanikio makubwa. Tunaingia mwaka 2026 tukiwa na miradi mingi yenye fursa za ukuaji na mwelekeo ulio wazi wa kuendelea kuzalisha faida bora na thamani endelevu kwa wanahisa wetu.

Ahsanteni sana.



_____

Peter William Kifunguomali
Afisa Mtendaji Mkuu

Tarehe: 21 Novemba 2026

TAARIFA YA UENDELEVU

utangulizi

Mafanikio ambayo Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE imeyapata kwa kuendeleza uwekezaji wenye uwajibikaji katika mwaka wa fedha 2025. Kufuatia mafanikio ya msingi yaliyopatikana mwaka 2024, tumeimarisha zaidi dhamira yetu ya kuzingatia **misingi ya Mazingira, Jamii na Utawala Bora (Environmental, Social and Governance – ESG)**, Kuhakikisha kuwa si viwango vya kupimia mafanikio tu, bali pia ni vichocheo muhimu vya uundaji wa thamani endelevu ya muda mrefu.

Uwajibikaji kwa mazingira: Kuelekea jalada la uwekezaji linalojali mazingira

Mwaka 2025, tulihama kutoka katika hatua za msingi za uhifadhi wa rasilimali na kuelekea katika urejeshaji wa mifumo ya ikolojia pamoja na kuelekeza mitaji kwenye uwekezaji wa kijani.

1. Usimamizi wa kisasa wa Nishati

- Kufuatia malengo tuliyojiwekea mwaka 2025, tulitekeleza **Mifumo ya Kisasa ya Usimamizi wa Nishati (Advanced Energy Management Systems – AEMS)** katika ofisi na majengo yetu ya biashara.
- Hatua hii ilisababisha kupungua kwa matumizi ya nishati kwa asilimia 10 zaidi, hivyo kuongeza ufanisi wa matumizi ya rasilimali na kupunguza athari kwa mazingira.

2. Mradi wa Upandaji Miti Mlima Kilimanjaro

- Katika mwaka huu, AFRIPRISE ilipanua kwa kiwango kikubwa mchango wake katika uhifadhi wa mazingira kwa kutoa msaada na kushirikiana na programu za upandaji miti katika maeneo ya miteremko ya Mlima Kilimanjaro.
- Mchango wetu uliwezesha upandaji wa miti ya asili ili kurejesha mfumo wa ikolojia wa mlima huo, kulinda vyanzo muhimu vya maji na kupunguza athari zinazotokana na kuyeyuka kwa barafu katika mlima huo.

Uwajibikaji kwa jamii: Kuwekeza katika uwezo wa rasilimali watu

Athari zetu kwa jamii katika mwaka 2025 zilielekezwa katika kuimarisha ustawi wa jamii na kukuza vipaji na uwezo wa wafanyakazi wetu.

Maendeleo ya wafanyakazi

Maendeleo ya Kitaaluma

- Tulianzisha **Mpango wa Ndani wa Ushauri wa Kitaaluma (Mentorship) na Uendelezaji wa Njia za Kazi (Career Pathing Program)**, unaowezesha **asilimia 100 ya wafanyakazi** kupata fursa za maendeleo ya kitaaluma na ukuaji wa kazi.

Ubora katika usawa na ujumuishi

- Tumeendelea kudumisha uwiano wa kijinsia wa asilimia 50 kwa 50 katika nguvu kazi yetu.
- Aidha, tumeongeza uwakilishi wa wanawake katika nafasi za uongozi wa juu, jambo linaloimarisha nafasi ya AFRIPRISE kama mwajiri anayezingatia usawa, ujumuishi na utofauti mahali pa kazi.

Utawala bora: Uadilifu na viwango vya juu vya uwajibikaji

Uwajibikaji, uwazi na maadili vinaendelea kuwa msingi mkuu wa uendeshaji wa shughuli zote za AFRIPRISE.

1. Kuimarisha Mfumo wa Tathmini ya ESG

- Tuliboresha **Mfumo wa Usimamizi wa Hatari za ESG**, kwa kuongeza vigezo madhubuti vya kupima **Athari za Kijamii (Social Impact).**
- Mfumo huu sasa unajumuisha ukaguzi wa kina wa mazingira ya kazi, haki za binadamu na viwango vya ajira kwa kila uwekezaji mpya unaotarajiwa kufanywa.

Mfumo wa Kupokea Maoni ya Wadau

- Tulianzisha mfumo mpya wa kidijitali wa ushirikishwaji wa wadau unaowezesha wawekezaji na wanajamii kutoa maoni yao moja kwa moja.
- Maoni hayo huchambuliwa na kuwasilishwa kwa Bodi ya Wakurugenzi kila robo mwaka kwa ajili ya kufanyiwa tathmini na kuchukuliwa hatua stahiki.

2. Uwekezaji unaofuata Maadili

- Maamuzi yetu yote ya uwekezaji yanaongozwa na mfumo madhubuti wa ESG unaohakikisha tunasaidia biashara zinazozingatia maadili mema ya biashara, uwajibikaji na uendelevu.
- Tunafanya tathmini za mara kwa mara za ESG kwa kampuni zilizopo katika jalada letu la uwekezaji ili kuhakikisha zinaendelea kuzingatia viwango vinavyotakiwa na kuboresha utendaji wake kila wakati.

3. Uwazi na Uwajibikaji

Tunazingatia viwango vya juu vya uwazi, uwajibikaji na utoaji wa taarifa kwa wakati kwa wanahisa, wawekezaji na wadau wengine wote. Kupitia mifumo yetu ya utawala bora, tunahakikisha kuwa maamuzi yote ya biashara yanafanywa kwa uadilifu, kwa kuzingatia sheria, kanuni na viwango bora vya kimataifa, huku tukijenga imani ya muda mrefu kwa wadau wetu wote.

- Tumeanzisha mfumo wa uwazi katika utoaji wa taarifa, unaowezesha wadau wetu kupata taarifa za mara kwa mara kuhusu maendeleo, utekelezaji na matokeo ya juhudi zetu za uendelevu.

Malengo ya Kimkakati ya Uendelevu kwa Kipindi cha 2026–2028	
Eneo	**Lengo la 2026–2028**
Mazingira	Kufikia kiwango cha kutozalisha kabisa kaboni katika shughuli zote za moja kwa
	moja za kampuni
Jamii	Kuzindua Mfuko wa "Ujasiriamali wa Kijani (Green Entrepreneurship Fund)"
	utakaotoa mtaji wa kuanzia (seed capital) kwa biashara changa za ndani
	zinazozingatia uendelevu.
Utawala Bora	Kupata uthibitisho huru wa ESG kutoka taasisi ya tatu (Third-Party ESG
	Certification) ili kuthibitisha kwa uhuru viashiria na utendaji wetu wa uendelevu.

TAARIFA YA BODI YA WAKURUGENZI

Wale wenye dhamana ya usimamizi wa kampuni (Wakurugenzi) wanafurahi kuwasilisha taarifa yao kuhusu Taarifa za Fedha za Kampuni ya Uwekezaji ya Umma ya AFRIPRISE ("Kampuni") kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2025. Taarifa hii inaelezea hali ya shughuli za Kampuni na utendaji wake katika mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2024 ambapo bei ya hisa ilikua shilingi 215 na 495 shilingi kwa 2025.

1. Usajili wa Kampuni

Kampuni ya Uwekezaji ya Afriprise imesajiliwa nchini Tanzania chini ya Sheria ya Kampuni ya mwaka 2002 kama kampuni ya umma yenye dhima yenye ukomo kwa hisa. Kampuni imeorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (Dar es Salaam Stock Exchange – DSE) na makao yake yako katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

2. Shughuli Kuu za Kampuni

Shughuli kuu za Kampuni ni usimamizi wa uwekezaji, zikijumuisha uwekezaji katika hisa za kampuni zilizoorodheshwa kwenye masoko ya mitaji, hati fungani za rejareja zinazotolewa na kampuni zenye historia ya faida endelevu, dhamana za Serikali pamoja na uwekezaji katika maghala yaliyopo katika maeneo ya kimkakati.

Aidha, Kampuni inahamasisha utamaduni wa kuweka akiba na uwekezaji miongoni mwa wanahisa wake kwa kuwekeza katika hisa za kampuni zenye utendaji mzuri na uwezo wa kuzalisha faida endelevu.

3. Maadili ya Msingi

Maadili yanayoongoza shughuli za Kampuni ni:

- Uwajibikaji;
- Kujitolea;
- Ushirikiano;
- Uaminifu; na
- Ubunifu.

MAONO, DHIMA, KAULI MBIU NA MAADILI KATIKA KAZI



DHAMIRA

Kuwaongezea wanahisa thamani ya muda mrefu kwa kutoa faida bora iliyozingatia usalama na uendelevu wa uwekezaji.



DIRA

Kuwa mtoa huduma bora wa usimamizi wa uwekezaji nchini Tanzania.



KAULI MBIU

"Pamoja tuna nguvu zaidi."

4. Mapitio ya Matokeo ya Kifedha na Shughuli za Kampuni

Taarifa za Fedha zimeandaliwa kwa kuzingatia **Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha (International Financial Reporting Standards – IFRS)** pamoja na matakwa ya **Sheria ya Kampuni ya mwaka 2002.** Sera za uhasibu zimetumika kwa uthabiti na bila mabadiliko ikilinganishwa na mwaka uliopita.

Kwa mwaka wa fedha 2025, Kampuni ilipata **faida halisi baada ya kodi ya TZS 4,520,821,000**, ikilinganishwa na **TZS 3,395,505,000** iliyopatikana mwaka 2024.

Mapato ya Kampuni kwa mwaka ulioishia tarehe **31 Desemba 2025** yaliongezeka na kufikia **TZS 5,118,532,000**, kutoka **TZS 4,219,666,000** mwaka uliopita, sawa na ongezeko la **asilimia 21**. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa mapato ya gawio, kufuatia uamuzi wa kimkakati wa Bodi ya Wakurugenzi wa kuendelea kuboresha na kutawanya jalada la uwekezaji wa Kampuni.

5. Mtaji wa Hisa

Mtaji wa Hisa Ulioidhinishwa

Aina ya Hisa	**2025**	**2024**		
Idadi ya Hisa za Kawaida Zilizoidhinishwa	5,000,000,000		5,000,000,000	
Mtaji wa Hisa Uliotolewa				
	2025	**2024**	**2025**	**2024**
Maelezo	(TZS '000)	(TZS '000)	Idadi ya Hisa	
Hisa za Kawaida	2,918,306	2,918,306	145,915,320	145,915,320
Akiba ya Ziada ya Mtaji	9,828,506	9,828,506	-	-
Jumla	**12,746,812**	**12,746,812**	**145,915,320**	**145,915,320**

Hakukuwa na mabadiliko yoyote katika mtaji wa hisa ulioidhinishwa wala uliotolewa katika kipindi cha mwaka kilichopita.

6. Gawio

Bodi ya Wakurugenzi inapendekeza kulipa kwa gawio la mwisho la TZS 23 kwa kila hisa, lenye jumla ya TZS 3,356,052,360.

Pendekezo hili ni ongezeko kutoka TZS 18 kwa kila hisa, sawa na TZS 2,626,475,760, zilizolipwa kwa wanahisa katika mwaka 2024.

7. Malengo ya Kimkakati

Bodi ya Wakurugenzi inaendelea kujizatiti kutekeleza mfumo madhubuti wa kimkakati unaolenga kuhakiki-sha ukuaji endelevu, ustahimilivu wa biashara na kuongeza thamani kwa wanahisa.

Mkakati wa Kampuni umejengwa juu ya nguzo sita kuu, ambazo zinaongoza utekelezaji wa malengo yetu ya muda mrefu:

I. Kuboresha Jalada la Uwekezaji na Ugawaji wa Mtaji

- **Uwakilishi wa PSSSF: Fortunatus Makore Magambo** na **Valentino Maganga** wanauwakilisha Mfuko wa

Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (Public Service Social Security Fund – PSSSF), ambao unamiliki hisa 65,661,894, sawa na asilimia 45 ya mtaji wa hisa uliotolewa wa Kampuni.

- **Uwakilishi wa TCCIA: CPA Vicent Bruno Minja** analiwakilisha Shirikisho la Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture – TCCIA), ambalo linamiliki hisa 701,333 katika Kampuni.

8. Utawala Bora wa Kampuni

Bodi ya Wakurugenzi ndiyo yenye jukumu la jumla la kusimamia shughuli za Kampuni. Majukumu yake yanajumuisha, pamoja na mengine, kubaini na kutathmini hatari zinazoweza kuathiri shughuli za Kampuni, kupitia na kufuatilia maamuzi makubwa ya uwekezaji, pamoja na kusimamia utekelezaji wa malengo ya kimkakati.

Aidha, Bodi ina wajibu wa kuhakikisha kuwa Kampuni ina mifumo, sera na taratibu madhubuti za udhibiti wa ndani ambazo ni kamilifu, zinafanya kazi kwa ufanisi na zinazingatia kanuni na misingi bora ya utawala wa kampuni.

Katika mwaka uliopita, Bodi ya Wakurugenzi ilifanya mikutano mitano (5), ambapo mikutano minne (4) ilikuwa ya kawaida na mkutano mmoja (1) ulikuwa wa dharura (Mkutano Maalumu), ulioitishwa kushughulikia masuala muhimu yaliyohitaji uamuzi wa haraka wa Bodi.

Bodi imekabidhi usimamizi wa shughuli za kila siku za Kampuni kwa Afisa Mtendaji Mkuu (Chief Executive Officer – CEO), ambaye anasaidiwa na timu ya menejimenti katika utekelezaji wa shughuli za Kampuni.

Menejimenti hualikwa kuhudhuria mikutano ya Bodi ili kutoa taarifa, ushauri wa kitaalamu na kuwezesha Bodi kusimamia kwa ufanisi shughuli za Kampuni.

Mkutano Maalumu wa Bodi ulijadili na kuidhinisha masuala muhimu, ikiwa ni pamoja na:

- Mpango wa Kazi wa Mwaka na Bajeti ya Kampuni;
- Taarifa za Fedha za Mwaka zilizokaguliwa;
- Miradi mipya ya uwekezaji; na
- Masuala mengine ya kimkakati yaliyohitaji maamuzi ya Bodi.

Tumeweka viwango madhubuti vya mgawanyo wa mali za uwekezaji ili kuhakikisha uwiano kati ya ukuaji wa thamani na uthabiti wa kifedha. Tunalenga kuelekeza **asilimia 50–65** ya uwekezaji katika hisa, na **asilimia 25–40** katika dhamana za Serikali.

Ili kupunguza athari za mabadiliko ya masoko, tunatekeleza mpango wa kurekebisha uwiano wa jalada la uwekezaji kila robo mwaka (Quarterly Portfolio Rebalancing), pamoja na kufanya majaribio ya uwezo wa kustahimili hatari (Stress Testing). Hatua hizi zinaungwa mkono na matumizi ya uchambuzi wa kisasa wa takwimu (Advanced Data Analytics) ili kuongeza usahihi wa maamuzi ya uwekezaji.

II. Ukuaji wa Mapato na Nidhamu katika Ugawaji wa Gawio

Kwa lengo la kuimarisha uwazi na uthabiti kwa wawekezaji wetu, Kampuni imepitisha sera rasmi ya gawio inayolenga kugawa kati ya **asilimia 50 hadi 70 ya Faida Baada ya Kodi iliyorekebishwa (Adjusted Profit After Tax – Adjusted PAT).**

Aidha, Kampuni inaelekeza mkazo katika kuongeza mapato endelevu yanayotokana na ada za ushauri, ada za usimamizi wa uwekezaji na huduma nyingine za kitaalamu. Mfumo wa motisha kwa menejimenti umeunganishwa na viashiria muhimu vya utendaji, hususan **Faida kwa Mtaji wa Wanahisa (Return on Equity – ROE) pamoja na Ukuaji wa Faida kwa Kila Hisa (Earnings Per Share – EPS).**

III. Upanuzi wa Kikanda na Ushirikiano wa Kimkakati

Kampuni inaendelea kutafuta kwa nguvu fursa za uwekezaji zenye matokeo makubwa katika ukanda wa **Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).**

Kila mwaka tunadumisha orodha ya fursa mbili hadi nne za uunganishaji wa kampuni au ubia wa kimkakati (Mergers & Acquisitions – M&A / Joint Ventures), huku tukitumia kiwango cha chini cha asilimia 15–18 cha Kiwango cha Ndani cha Faida ya Uwekezaji (Internal Rate of Return – IRR) kama kigezo cha tathmini.

Kipaumbele kinatolewa katika sekta zenye mchango mkubwa kwa maendeleo ya kikanda, ikiwemo:

- Uchakataji wa mazao ya kilimo;
- Usafirishaji na ugavi (Logistics); na
- Huduma za viwanda.

IV. Usimamizi wa Hatari, ESG na Ukwasi

Mfumo wetu wa utawala bora sasa umeunganisha kikamilifu vigezo vya **Mazingira, Jamii na Utawala Bora (Environmental, Social and Governance – ESG)** katika maamuzi yote ya uwekezaji.

Tunadumisha kiwango bora cha ukwasi kwa kuhakikisha Kampuni inakuwa na fedha taslimu za kuendesha shughuli kwa angalau siku 120. Lengo hili linaungwa mkono na utabiri wa mtiririko wa fedha unaofanyika kila mwezi pamoja na Daftari la Hatari (Risk Register) linaloboreshwa kila robo mwaka ili kulinda mali na maslahi ya Kampuni.

V. Ubora wa Uendeshaji na Mageuzi ya Kidijitali

Tunaendelea kuwekeza katika uboreshaji wa mifumo ya ndani kupitia matumizi ya teknolojia na uendeshaji wa kiotomatiki (Automation), pamoja na kuboresha mifumo ya kidijitali ya usimamizi wa jalada la uwekezaji.

Hatua hizi zinalenga:

Kuboresha usahihi wa taarifa na ripoti;
Kuimarisha usalama wa mifumo ya taarifa (Cybersecurity);
Kuongeza uwezo wa ndani wa kubuni bidhaa changamani za kifedha; na
Kuimarisha usimamizi wa hatari kwa kutumia teknolojia za kisasa.

VI. Ubunifu na Ushiriki katika Soko

Kampuni inaendelea kuwa kinara katika ubunifu wa bidhaa za kifedha kwa kuendeleza bidhaa za uwekezaji zilizoundwa mahsusi (Structured Products) pamoja na suluhisho za kifedha kwa Biashara Ndogo na za Kati (SMEs) zinazolingana na vipaumbele vya maendeleo ya taifa.

Aidha, tumejizatiti kuongeza mwonekano wetu katika soko kupitia mikutano ya mara kwa mara na wawekezaji (Investor Roadshows), pamoja na matumizi ya njia mbalimbali za mawasiliano ya kidijitali. Hatua hizi zinalenga kuhakikisha uwazi, ushirikishwaji na mawasiliano endelevu na wanahisa pamoja na wadau wote wa Kampuni.

9. Malengo ya Kimkakati

Bodi ya Wakurugenzi inaendelea kutekeleza mfumo madhubuti wa kimkakati unaolenga kuhakikisha ukuaji endelevu, ustahimilivu wa biashara na kuongeza thamani kwa wanahisa.

10. Bodi ya Wakurugenzi

Jina la Mkurugenzi	Wadhifa	Taaluma	Uraia
Fortunatus Makore Magambo	Mwenyekiti	Mchumi	Mtanzania
Prof. Lucian A. Msambichaka	Mjumbe	Mchumi	Mtanzania
Joseph Matanga Kahungwa	Mjumbe	Mhasibu	Mtanzania
Magdalene N. E. Mkocha	Mjumbe	Mchumi wa Kilimo	Mtanzania
Nathan E. Mnyawami	Mjumbe	Mchumi	Mtanzania
CPA. Vicent Minja	Mjumbe	Mhasibu	Mtanzania
Adv. Valentino Daudi	Mjumbe	Mwanasheria	Mtanzania

11. Matukio Baada ya Kipindi cha Taarifa za Fedha

Kwa mujibu wa taratibu na viwango vya kawaida vya uandaaji wa taarifa za fedha, Wakurugenzi wanathibitisha kuwa hakujatokea tukio lolote muhimu baada ya tarehe ya mwisho wa mwaka wa fedha hadi tarehe ya taarifa hii ambalo lingehitaji kurekebishwa au kutolewa taarifa katika Taarifa za Fedha.

12. Katibu wa Kampuni

Hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2025, **Peter William Kifunguomali** aliendelea kuhudumu kama **Katibu wa Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE.**

13. Michango ya Kisiasa na Misaada ya Kijamii

Kama sehemu ya utekelezaji wa dhamira yetu ya Mazingira, Jamii na Utawala Bora (ESG), Kampuni ilichangia na kushiriki katika kampeni ya upandaji miti mwaka 2025 kwa lengo la kusaidia urejeshaji wa mifumo ya ikolojia na uhifadhi wa mazingira.

Hatua hii inaashiria mwelekeo mpya wa kimkakati ikilinganishwa na mwaka 2024, ambapo Kampuni haikutoa michango yoyote ya misaada ya kijamii.

Aidha, tunathibitisha kuwa hakuna fedha zozote za Kampuni zilizotumika kwa michango ya kisiasa, kwa kuzingatia sera na misingi ya utawala bora ya Kampuni.

14. Usimamizi wa Hatari na Udhibiti wa Ndani

Kampuni inatekeleza mfumo jumuishi wa usimamizi wa hatari ulioundwa kubaini, kutathmini na kudhibiti vihatarishi vinavyoweza kuathiri utekelezaji wa malengo yetu ya kimkakati.

Umiliki wa Hisa za Wakurugenzi Katika Kampuni

Jina la Mkurugenzi	2025	2024
	Umiliki	Umiliki
Prof. Lucian A. Msambichaka	131,760	131,760
Joseph Matanga Kahungwa	81,200	81,200
Magdalene N. E. Mkocha	204,724	204,724
Nathan E. Mnyawami	42,150	42,150
	459,834	459,834

Mfumo huu unahakikisha kuwa maamuzi yote yanayohusisha hatari yanafanywa kwa makusudi, kwa uwazi na kwa kuzingatia lengo la kuongeza thamani endelevu kwa wanahisa katika kipindi cha muda mrefu.

Hatari za Soko na Viwango vya Riba

Asili ya Hatari

Hatari hizi zinajumuisha:

- Mabadiliko ya thamani za uwekezaji katika hisa na hati fungani;
- Mabadiliko ya viwango vya riba katika soko; na
- Mabadiliko ya mapato yanayotokana na shughuli za utoaji wa mikopo na uwekezaji.

Mikakati ya Kudhibiti Hatari

Ili kupunguza athari za vihatarishi hivyo, Kampuni:

- Inazingatia sera madhubuti ya uwekezaji inayosisitiza **utawanyaji wa uwekezaji (asset diversification)**;
- Hufanya **marekebisho ya uwiano wa jalada la uwekezaji (portfolio rebalancing)** kulingana na mabadiliko ya soko;
- Hufanya **majaribio ya uwezo wa kustahimili hatari (stress testing)** mara kwa mara; na
- Hutekeleza viwango madhubuti vya udhibiti wa hatari (risk limits) ili kulinda mtaji wa Kampuni na kuhakikisha uthabiti wa utendaji wake hata wakati wa mabadiliko makubwa ya soko.

15. Umiliki wa Hisa za Wakurugenzi Katika Kampuni

Kufikia tarehe 31 Desemba 2025, maslahi ya moja kwa moja ya umiliki wa hisa yaliyokuwa yakimilikiwa na Wakurugenzi katika mtaji wa hisa uliotolewa wa Kampuni ni kama yanavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:

Wajumbe wote wa Bodi ya Wakurugenzi wanatambuliwa na Bodi kuwa ni huru katika maamuzi na mwenendo wao, wenye uwezo wa kutoa maamuzi kwa weledi na bila kuathiriwa na maslahi binafsi, mahusiano au mazingira yoyote yanayoweza kuathiri uhuru wa maamuzi yao.

Bodi ya wakurugenzi na mahudhurio katika mwaka 2025;

Wakurugenzi	Nafasi / Cheo	Jumla ya Vikao	Idadi ya Vikao Vilivyohudhuriwa
Fortunatus Makore Magambo	Mwenyekiti	5	4
Prof. Lucian A. Msambichaka	Mjumbe	5	5
Joseph Matanga Kahungwa	Mjumbe	5	5
Magdalene N. E. Mkocha	Mjumbe	5	5
Nathan E. Mnyawami	Mjumbe	5	4
Adv. Valentino Daudi	Mjumbe	5	4
CPA. Vicent Minja	Mjumbe	5	4
Mr. Peter W. Kifunguomali	Katibu	5	5

Aidha, Bodi inaamini kuwa Wakurugenzi wote wameendelea kutekeleza majukumu yao ya uaminifu (fiduciary duties) kwa kuzingatia viwango vya juu vya maadili, uadilifu na uwajibikaji katika kipindi chote cha mwaka uliopita.

Bodi ya Wakurugenzi inatambua umuhimu wa kuzingatia kanuni za utawala bora wa kampuni na inaendelea kujizatiti kuhakikisha kanuni hizo zinazingatiwa katika shughuli zote za Kampuni.

Katika mwaka uliopita, Bodi ilitumia Kamati mbili za Bodi ili kuimarisha utekelezaji wa misingi ya utawala bora, kuongeza ufanisi katika usimamizi wa Kampuni na kuwezesha maamuzi muhimu kufanyika kwa wakati.

Kamati hizo ni:

Kamati ya Uwekezaji, yenye wajumbe watatu (3); na
Kamati ya Ukaguzi na Usimamizi wa Hatari, yenye wajumbe watatu (3).

Kamati ya Uwekezaji

Kamati ya Uwekezaji iliundwa na wajumbe wafuatao:

Jina	**Wadhifa**
Prof. Lucian A. Msambichaka	**Mwenyekiti**
Nathan E. Mnyawami	**Mjumbe**
Adv. Valentino Daudi	**Mjumbe**

Katika mwaka uliopita, Kamati ya Uwekezaji ilifanya mikutano minne (4) kwa ajili ya kupitia na kujadili taarifa za utendaji za kila robo mwaka pamoja na mapendekezo ya uwekezaji, kabla ya kuyawasilisha kwa Bodi ya Wakurugenzi kwa ajili ya majadiliano na maamuzi.

Kamati ya Ukaguzi na Usimamizi wa Hatari

Kamati ya Ukaguzi na Usimamizi wa Hatari iliundwa na wajumbe wafuatao:

Jina	Wadhifa
Joseph M. Kahungwa	**Mwenyekiti**
Magdalene N. E. Mkocha	**Mjumbe**
CPA. Vicent Minja	**Mjumbe**

16. Utawala Bora wa Kampuni

Kamati ya Ukaguzi na Usimamizi wa Hatari ilifanya mikutano minne (4) katika mwaka uliopita kwa ajili ya kujadili na kupitisha taarifa za ukaguzi wa ndani za kila robo mwaka zilizokuwa zimeandaliwa na Mkaguzi wa Ndani. Aidha, Kamati ilipitia na kujadili rasimu ya Taarifa za Fedha za Mwaka kabla ya kuziwasilisha kwa Bodi ya Wakurugenzi kwa ajili ya kuidhinishwa.

Usimamizi wa Kimkakati wa Bodi

Katika mwaka 2025, Bodi ya Wakurugenzi ilielekeza juhudi zake katika kukamilisha utekelezaji wa Mpango Mkakati wa miaka 2023–2025, pamoja na kuidhinisha Mpango Mkakati wa miaka 2026–2028 unaolenga kuleta mageuzi makubwa katika shughuli za Kampuni.

Mpito huu unaashiria mabadiliko ya Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE kutoka kampuni ya kawaida ya uwekezaji kwenda kuwa taasisi ya kifedha ya kikanda yenye shughuli mbalimbali na ushindani mkubwa.

Uidhinishaji wa Mkakati wa Miaka 2026–2028

Bodi iliidhinisha Mpango Mkakati mpya wa miaka mitatu unaojengwa katika maeneo makuu yafuatayo:

- Uimarishaji wa Muundo wa Mtaji: Bodi iliidhinisha utoaji wa Hisa za Upendeleo za daraja A zisizo na haki ya kupiga kura, zinazoweza kukombolewa na zenye haki ya gawio linalokusanywa (Series A Non-Voting Redeemable Cumulative Preference Shares), ili kupata mtaji wa muda mrefu kwa ajili ya kugharamia miradi yenye athari kubwa za kiuchumi.

- **Upanuzi wa Kikanda:** Bodi ilielekeza Kampuni kuongeza uwekezaji na kupanua shughuli zake katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Tathmini ya Utekelezaji wa Mkakati wa Miaka 2023–2025

Mapitio ya kina ya utekelezaji wa Mpango Mkakati uliomalizika yalionyesha mafanikio makubwa katika utendaji wa kifedha na shughuli za Kampuni, ikiwa ni pamoja na:

- **Kuongezeka kwa Faida:** Kampuni ilifanikiwa kuongeza faida halisi baada ya kodi kutoka TZS bilioni 1.98 mwaka 2023, hadi TZS bilioni 3.40 mwaka 2024, na kufikia TZS bilioni 4.52 mwaka 2025.
- **Ukuaji wa Mapato:** Mapato ya Kampuni yaliongezeka kwa asilimia 37 mwaka 2024, na kufikia TZS bilioni 4.22. Mwaka 2025, mapato yaliendelea kuongezeka kwa asilimia 21, na kufikia TZS bilioni 5.11.
- **Kuimarika kwa Mtaji:** Kampuni ilisimamia kwa mafanikio zoezi la kuongeza mtaji kupitia Rights Issue lenye thamani ya TZS bilioni 10, ambalo liliongeza kwa kiasi kikubwa mtaji wa hisa uliotolewa.
- **Mabadiliko ya Utambulisho wa Kampuni:** Kampuni ilikamilisha kwa mafanikio mchakato wa kubadilisha jina na utambulisho wake kuwa Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE, na kujijengea chapa ya kisasa

yenye mtazamo wa bara la Afrika (Pan-African Brand).

Mtazamo wa Kimkakati na Uchambuzi wa Mapengo (Gap Analysis)

Bodi ilitumia uchambuzi wa mapengo (Gap Analysis) kama nyenzo muhimu ya kuimarisha mfumo wa utawala bora na kupanga hatua za maendeleo ya baadaye.

Matokeo ya uchambuzi huo yaliainisha maeneo yafuatayo kuwa vipaumbele vya kimkakati:

- **Kuimarisha Ustahimilivu wa Hatari:** Bodi ilitoa kipaumbele kwa ujumuishaji wa kina wa viwango vya Mazingira, Jamii na Utawala Bora (ESG) katika shughuli zote za Kampuni, pamoja na kuimarisha usimamizi wa ukwasi kwa kuhakikisha Kampuni inakuwa na fedha taslimu za kuendesha shughuli kwa angalau siku 120.
- **Kuimarisha Utawala Bora:** Bodi ilithibitisha kuwa msingi imara wa mtaji pamoja na muundo ulioboreshwa wa Kampuni vinatoa uwezo na uthabiti unaohitajika ili kutekeleza mkakati wa upanuzi wa shughuli za Kampuni katika ngazi ya kikanda.

17. Uzingatiaji wa Sheria na Kanuni

Katika mwaka uliopita, Kampuni ilitekeleza na kuzingatia kikamilifu wajibu wake wote wa kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Kampuni ya Tanzania ya mwaka 2002, pamoja na kanuni na matakwa mengine yote yanayosimamia shughuli za kampuni za umma na taasisi za uwekezaji nchini Tanzania.

Katika mwaka uliopita, Kampuni ilitekeleza kikamilifu wajibu wake wote wa kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Kampuni ya Tanzania ya mwaka 2002.

Aidha, Kampuni iliendelea kuzingatia kwa ukamilifu miongozo na kanuni zinazotolewa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (Capital Markets and Securities Authority – CMSA) pamoja na Soko la Hisa la Dar es Salaam (Dar es Salaam Stock Exchange – DSE).

Vilevile, Kampuni ilizingatia kikamilifu sheria zote za kodi na kanuni zinazotekelezwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (Tanzania Revenue Authority – TRA) kwa kuhakikisha kuwa marejesho yote ya kodi yaliwasilishwa kwa wakati na malipo yote ya kodi yalifanyika kwa mujibu wa sheria. Hatua hii imeendelea kuimarisha uadilifu wa Kampuni katika Soko la Hisa na kulinda maslahi ya wanahisa pamoja na wadau wengine wote.

18. Uaminifu wa Rekodi za Uhasibu na Taarifa za Fedha

Kampuni ina timu yenye sifa, ujuzi na uzoefu katika idara ya Uhasibu na Fedha. Kutokana na hilo, vitabu vya hesabu vimehifadhiwa na kusimamiwa ipasavyo kwa kuzingatia viwango vinavyotakiwa.

Taarifa za Fedha zimeandaliwa kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha (International Financial Reporting Standards – IFRS), ili kuhakikisha zinatoa taarifa sahihi, za kuaminika na zinazoakisi hali halisi ya kifedha ya Kampuni.

19. Muundo wa Mtaji wa Kampuni

Kufikia tarehe 31 Desemba 2025, mtaji wa hisa ulioidhinishwa wa Kampuni uliendelea kuwa TZS bilioni 100. Mtaji huu unajumuisha hisa za kawaida 5,000,000,000, ambapo kila hisa ina thamani ya kawaida (par value) ya TZS 20.

	2025 TZS '000	2024 TZS '000
Zilizoidhinishwa		
Hisa za kawaida 5,000,000,000 za TZS 20 kila moja	100,000,000	100,000,000
Zilizotolewa, zilizosajiliwa na kulipiwa		
Hisa za kawaida 145,915,320 (2024: 145,915,320)		
za TZS 20 kila moja	2,918,306	2,918,306
Sifa ya ziada ya hisa (Share premium)	9,828,506	9,828,506
	12,746,812	**12,746,812**

Muundo wa Umiliki wa Hisa (Shareholding Structure)

Muundo wa Umiliki wa Hisa	**Hisa Zilizoshikiliwa**		**Asilimia ya Hisa**	**TZS '000**
PSSSF	65,661,894	45.00%		1,313,238
Abbasi Exports Limited	17,639,158	12.10%		352,783
Joyce Mwita Gachuma	14,423,911	9.90%		288,478
Amin Mohamed Valji	2,110,000	1.40%		42,200
iGrowth Managed Fund	1,616,420	1.10%		32,328
Fayaz Feroz Rashid	1,236,400	0.80%		24,728
Other Shareholders (less than 1.5)	43,227,537	29.60%		864,551
Jumla	**145,915,320**	**100%**		**2,918,306**

20. Taarifa za soko la hisa

Bodi inayo furaha kuwataarifu kuhusu ongezeko kubwa la thamani ya hisa, jambo lililodhihirishwa na ongezeko la 230% la bei ya hisa tangu Desemba 2022 na Kufikia TZS 495 Desemba 2025. Kwa sasa hisa zinauzwa kwa thamani iliyo juu ya thamani halisi ya mali za Kampuni (Net Asset Value - NAV). Tunahusisha mabadiliko haya ya kimsingi ya soko na utekelezaji mzuri wa nguzo zetu za kimkakati, ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya Kuwa Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE, ulipaji kamili wa mikopo yote ya benki, na upatikanaji wa ukuaji mkubwa wa mapato.

21. Biashara endelevu na Usimamizi wa Mazingira

Katika Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE, tunaamini kwamba uundaji wa thamani ya muda mrefu unashabihiana kikamilifu na uendelevu wa mifumo ya ikolojia na jamii tunazofanyia kazi. Mnamo 2025, tulitoka kwenye mbinu ya kujihami ya usimamizi wa riski na kuhamia kwenye mkakati thabiti wa uwekezaji unaoongozwa na misingi ya ESG (Mazingira, Jamii na Utawala), tukihakikisha kwamba mtaji wetu unatengwa kwa taasisi zenye rekodi zilizothibitishwa za utunzaji wa mazingira na usalama. Ishara kuu ya utendaji wetu mwaka huu ilikuwa ni mchango wetu katika kampeni ya kitaifa ya kupanda miti, hatua ya kimkakati ya kufidia athari za kiutendaji za kampuni yetu na kuunga mkono malengo ya kitaifa ya upandaji miti upya.

Aidha, tumefanikiwa kurasimisha mazingira ya utoaji taarifa bila kutumia karatasi kwa kupitisha mifumo ya kidijitali ya usimamizi wa uwekezaji, na hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa taka ngumu. Kwa kuunganisha vigezo vya ESG katika uhakiki wa kina wa uwekezaji wetu (due diligence) na kutoa kipaumbele kwa

teknolojia zinazozingatia mabadiliko ya tabianchi ("climate-smart"), tunahakikisha kuwa AFRIPRISE inasalia kuwa chachu ya mabadiliko endelevu ya kijamii na kiuchumi kote Afrika.

22. Taarifa ya uendelevu wa kampuni (Going concern statement)

Wakurugenzi wamepitia hali ya kifedha ya kampuni na wana imani kwamba Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE ina rasilimali za kutosha kuendeleza shughuli zake za kiutendaji kwa siku zijazo zinazoonekana. Tathmini hii inaungwa mkono na wasifu thabiti wa ukwasi wa kampuni, ikiwa ni pamoja na akiba ya fedha taslimu inayoweza kukidhi mahitaji ya siku 120 (120-day cash-on-hand buffer) na mkakati wa kuondoa mikopo mikubwa ya benki.

Taarifa za kifedha zimeandaliwa kwa msingi wa kampuni kuendelea kuwepo (going concern basis), kwani wakurugenzi wana matarajio ya kuridhisha kwamba kampuni ina uwezo wa kupata huduma na fursa za kutosha ili kutimiza ahadi zake za uwekezaji na majukumu ya kiutawala.

Bodi haina taarifa juu ya ukiukwaji wowote mkubwa wa mahitaji ya kisheria au mabadiliko ya kisheria yanayosubiriwa ambayo yangewezesha kuathiri vibaya uwezo wa kampuni wa kuendeleza shughuli zake.

23. Ustawi wa Wafanyakazi

Inajumuisha ufadhili wa mafunzo, mikopo/mishahara ya mapema (advances) kwa wafanyakazi, misaada ya kifedha ya msiba, michango ya kustaafu ya PSSSF, na bima ya afya kupitia NHIF. Mpaka kufikia tarehe 31 Desemba 2025, kampuni ilikuwa na wafanyakazi 6 (wanaume 3, wanawake 3).

24. Usawa wa Jinsia na Ujumuishi

Kampuni inaamini kuwa kila mfanyakazi anapaswa kupewa fursa sawa bila kujali jinsia.
Kampuni inahakikisha wanawake na wanaume wanashiriki kwa uwiano katika ajira. Mpaka kufikia tarehe 31 Desemba 2025, Kampuni imefanikiwa kudumisha usawa wa kijinsia kwa wafanyakazi, huku wanawake wakichangia 50% ya wafanyakazi wote. Ahadi hii ya usawa wa kijinsia inaonekana pia katika ngazi za juu kabisa za uongozi kupitia uwakilishi mkubwa wa wanawake kwenye Bodi ya Wakurugenzi.

25. Taarifa ya Mazingira, Jamii na Utawala (ESG)

Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE inaendelea kutambua kwa kina athari zake kwa jamii na mazingira, ikihakikisha kwamba misingi ya ESG inaunganishwa katika kila nyanja ya uendeshaji wa shughuli zetu.

26. Shughuli za maendeleo ya baadaye

Bodi inaendelea kubadili na kupanua uwekezaji wake (diversify) katika dhamana za kifedha za mapato yaliyowekwa kima (fixed-income instruments), kama vile dhamana za serikali. Pia, inachunguza sekta mpya zikiwemo za viwanda, uingizaji na usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi (import/export), na biashara ya hatifani (bond trading).

27. Kulinda Rasilimali za Kampuni

Wakurugenzi ndio wenye jukumu la msingi la kulinda na kuhifadhi mali na rasilimali za kampuni. Ili kuhakikisha mazingira salama ya kiutendaji, Bodi imeidhinisha sera mbalimbali, zikiwemo kanuni za kifedha

na sera za uwekezaji, ambazo hufanyiwa mapitio mara kwa mara ili ziendane na mabadiliko ya soko.

Mambo makuu ya kuzingatia kuhusu ulindaji wa rasilimali ni pamoja na:

- **Mazingira ya Udhibiti wa Ndani:** Kampuni inatumia sera mbalimbali ili kuimarisha mazingira yake ya udhibiti na kudhibiti riski.
- **Usimamizi wa Ukaguzi:** Shughuli za ukaguzi wa ndani zilizokasimishwa kwa kampuni ya nje (outsourced) hutoa taarifa kwa Kamati ya Ukaguzi ya Bodi ili kufuatilia na kuelekeza hatua za kurekebisha mapungufu.
- **Uadilifu wa Rasilimali:** Hakuna matukio yoyote makubwa ya udanganyifu (wizi/ufisadi) yaliyoripotiwa katika mwaka unaoangaziwa.
- **Mageuzi ya Sera:** Uongozi unadumisha udhibiti thabiti wa ndani kupitia miongozo ya kiutendaji iliyohuishwa, kanuni, na sera za kiutaratibu.

28. Miamala ya pande zinazohusiana (Related party transactions)

Kulingana na ahadi yetu ya uwazi na uzingatiaji wa sheria, mchanganuo wa kina wa miamala yote ya pande zinazohusiana na bakaa za mwisho wa mwaka umetolewa katika Kumbukumbu namba 34 ya taarifa za kifedha.

29. Jukumu la Bodi na Uidhinishaji

Wakurugenzi wanathibitisha kwamba taarifa za kifedha zinaonyesha kwa ukweli na haki hali halisi ya Kampuni na zinazingatia viwango vyote vinavyohusika vya utoaji taarifa. Taarifa za kifedha katika kurasa za 19 hadi 53 ziliidhinishwa na Bodi mnamo Tarehe 30 Mei, 2026 na zimesainiwa kwa niaba yake na:

_____

Fortunatus Makore Magambo
Mkurugenzi

Tarehe: 30 Mei, 2026

_____

Prof. Lucian A. Msambichaka
Mkurugenzi

Tarehe: 30 Mei, 2026

TAARIFA YA MKUU WA IDARA YA UHASIBU WA KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA AFRIPRISE

Tamko la Mkuu wa Kitengo cha Fedha/Uhasibu wa Kampuni ya Uwekezaji ya Afriprise

Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA), kwa mujibu wa mamlaka iliyopewa chini ya Sheria ya Usajili wa Wakaguzi na Wahasibu Na. 33 ya mwaka 1972, kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 2 ya mwaka 1995, inataka taarifa za kifedha ziambatane na tamko lililotolewa na Mkuu wa Kitengo cha Fedha/Uhasibu mwenye dhamana ya uandaaji wa taarifa za kifedha za taasisi husika.

Ni wajibu wa Mhasibu wa Kitaalamu kuisaidia Bodi ya Wakurugenzi/Mamlaka Inayoongoza/Uongozi kutekeleza majukumu ya kuandaa taarifa za kifedha za taasisi zinazoonyesha taswira halisi na ya haki ya hali ya kifedha na utendaji wa taasisi hiyo, kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu vinavyohusika na mahitaji ya kisheria ya utoaji wa taarifa za kifedha.

Wajibu kamili wa kisheria wa uandaaji wa taarifa za kifedha unajumuishwa kwa Bodi ya Wakurugenzi/Mamlaka Inayoongoza kama ilivyoelezwa chini ya Taarifa ya Majukumu ya Wakurugenzi katika ukurasa uliopita.

Mimi, Joel Chikoma, nikiwa Mkuu wa Kitengo cha Fedha/Uhasibu wa Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE kufikia tarehe 31 Desemba 2025 na kwa mwaka ulioishia tarehe hiyo, nakiri wajibu wangu wa kuhakikisha kwamba taarifa za kifedha kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2025 zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango vya uhasibu vinavyohusika na mahitaji ya kisheria.

Hivyo basi, nathibitisha kwamba taarifa hizi za kifedha zinaonyesha taswira halisi na ya haki ya hali ya kifedha ya Kampuni ya Uwekezaji ya AFRIPRISE kufikia tarehe hiyo, na kwamba zimeandaliwa kwa kuzingatia kumbukumbu za kifedha zinazotunzwa ipasavyo.

Jina: CPA. Joel Chikoma

Saini: _____

Wadhifa: Mkuu wa Kitengo cha Fedha
Namba ya Uanachama wa NBAA: ACPA 3285

Tarehe: 30 Mei, 2026



TAARIFA YA MAHESABU

	Kumb	2025 TZS '000	2024 TZS '000
Rasilimali (Mali)			
Rasilimali zisizohamishika / Zisizo za sasa			
Majengo, mitambo na vifaa	4	**222,835**	115,766
Nyumba au ardhi ya uwekezaji	5	**212,112**	
Haki ya matumizi ya rasilimali	8	**74,578**	40,553
Rasilimali zisizoshikika	6	**-**	1,027
Mikopo inayodaiwa	7	**-**	47,957
Uwekezaji wa hisa	10	**44,660,751**	30,949,793
Uwekezaji katika dhamana za serikali	9	**11,823,898**	15,680,721
Rasilimali zingine za kifedha	12	**1,700,000**	1,200,000
		58,694,174	48,247,929
Rasilimali za sasa			
Mikopo inayodaiwa	7	**54,241**	36,340
Biashara na madeni mengine yanayodaiwa	14	**1,635,656**	669,164
Kodi ya sasa inayodaiwa		**350,857**	333,423
Rasilimali zingine za kifedha	12	**1,442,672**	1,155,000
Fedha taslimu na kiasi sawa na fedha taslimu	15	**670,593**	2,241,156
		4,154,019	4,435,083
Jumla ya Rasilimali		**62,848,193**	52,683,012
Mtaji na Madeni			
Mtaji			
Mtaji wa hisa	16	**12,746,812**	12,746,812
Akiba ya kifedha		**23,172,051**	14,912,266
Faida iliyolundikwa / Mapato yaliyobaki		**26,783,756**	24,889,411
		62,702,619	52,548,489
Madeni			
Madeni ya muda mrefu / Zisizo za sasa			
Kodi iliyeahirishwa	13	**1,784**	1,784
Deni la pango	17	**-**	-
		1,784	1,784
Madeni ya sasa / Muda mfupi			
Biashara na madeni mengine yanayopaswa kulipwa	18	**25,724**	36,539
Gawio linalopaswa kulipwa	19	**43,488**	47,406
Deni la pango	17	**74,578**	48,794
		143,790	132,739
Jumla ya Madeni		**145,574**	134,523
Jumla ya Mtaji na Madeni		**62,848,193**	52,683,012

	Kumb	2025 TZS '000	2024 TZS '000
Mapato	**20**	**5,118,532**	4,219,666
Mapato mengine ya uendeshaji	**21**	**1,002,111**	466,937
Gharama za miamala ya mtaji	**22**	**(18,507)**	-
Gharama za uendeshaji	**23**	**(1,439,740)**	(1,172,578)
Faida ya uendeshaji		**4,662,396**	3,514,025
Gharama za fedha	**26**	**(2,335)**	(10,079)
Faida kabla ya kodi		**4,660,061**	3,503,946
Kodi	**27**	**(139,240)**	(108,441)
Faida kwa mwaka		**4,520,821**	3,395,505
Mapato mengine jumuishi:			
Mapato mengine jumuishi ya mwaka baada ya kodi			
Faida kutokana na utathamini wa uwekezaji katika zana za mtaji		**8,259,785**	3,533,903
Mapato mengine jumuishi ya mwaka baada ya kodi		**8,259,785**	3,533,903
Jumla ya mapato jumuishi kwa mwaka		**12,780,606**	6,929,408
Pato la msingi na lililopunguzwa kwa kila hisa	**2**	**30.98**	23.33

	Mtaji wa Hisa	Ziada ya Hisa	Jumla ya Mtajiwa Hisa	Akiba ya Tathmini ya Thamani Halisi	Gharama za IPO	Jumla ya Akiba na Gharama za IPO	Mapato Yaliyobakizwa	Jumla ya Hisa za Wamiliki
	TZS '000	TZS '000	TZS '000	TZS '000	TZS '000	TZS '000	TZS '000	TZS '000
Salio1 Januari 2024	2,918,306	9,828,506	12,746,812	13,788,914	(1,229,088)	12,559,826	22,218,290	47,524,928
Faida ya mwaka	-	-	-	-	-	-	3,395,505	3,395,505
Mapato mengine ya kina	-	-	-	3,533,903	-	3,533,903	-	3,533,903
Jumla ya mapato ya kina kwa mwaka	**2,918,306**	**9,828,506**	**12,746,812**	**17,322,817**	**(1,229,088)**	**16,093,729**	**25,613,795**	**6,929,408**
Uhamisho kati ya akiba	-	-	-	(1,181,463)	-	(1,181,463)	1,181,463	-
Gawio	-	-	-	-	-	-	(1,905,847)	(1,905,847)
Jumla ya mabadiliko	-	-	-	(1,181,463)	-	(1,181,463)	(724,384)	(1,905,847)
Salio tarehe 31 Desemba 2024	**2,918,306**	**9,828,506**	**12,746,812**	**16,141,354**	**(1,229,088)**	**14,912,266**	**24,889,411**	**52,548,489**
Salio tarehe 1 Januari 2025	2,918,306	9,828,506	12,746,812	16,141,354	(1,229,088)	14,912,266	24,889,411	52,548,489
Faida ya mwaka	-	-	-	-	-	-	4,520,821	4,520,821
Mapato mengine ya kina	-	-	-	8,259,785	-	8,259,785	-	8,259,785
Jumla ya mapato ya kina kwa mwaka	**2,918,306**	**9,828,506**	**12,746,812**	**24,401,139**	**(1,229,088)**	**23,172,051**	**29,410,232**	**65,329,095**
Uhamisho kati ya akiba	-	-	-		-	-	-	-
Gawio	-	-	-	-	-	-	(2,626,476)	(2,626,476)
Jumla ya mabadiliko	-	-	-	-	-	-	(2,626,476)	(2,626,476)
Salio tarehe 31 Desemba 2025	**2,918,306**	**9,828,506**	**12,746,812**	**24,401,139**	**(1,229,088)**	**23,172,051**	**26,783,756**	**62,702,619**
Kumb	16	16	16					

	Kumb	2025 TZS '000	2024 TZS '000
Mtiririko wa Fedha kutoka Shughuli za Uendeshaji			
Fedha taslimu zilizotokana na shughuli za uendeshaji	**28**	**3,771,144**	3,786,230
Gharama za fedha		**(2,335)**	(10,079)
Kodi iliyolipwa	**29**	**(156,673)**	(133,700)
Jumla ya fedha taslimu zilizotokana na shughuli za uendeshaji		**3,612,136**	3,642,451
Mtiririko wa Fedha kutoka Shughuli za Uwekezaji			
Ununuzi wa mali, mitambo na vifaa	**4**	**(151,543)**	(37,467)
Mauzo ya mali za uwekezaji	**5**	**-**	9,235
Upatikanaji wa mali za haki ya matumizi	**8**	**(74,578)**	(74,866)
Uuzaji wa mali za haki ya matumizi	**8**	**-**	57,322
Uwekezaji katika dhamana za Serikali		**3,856,823**	(642,845)
Mabadiliko katika uwekezaji wa hisa		**(13,710,958)**	(5,592,550)
Mabadiliko katika mikopo inayodaiwa		**30,056**	17,830
Upatikanaji wa uwekezaji mwingine		**(787,674)**	(1,300,000)
Mapato halisi kutokana na uuzaji wa uwekezaji wa hisa		**8,259,785**	3,533,904
Jumla ya fedha taslimu zilizotumika katika shughuli za uwekezaji		**(2,578,089)**	(4,029,437)
Mtiririko wa Fedha kutoka Shughuli za Ufadhili			
Mabadiliko katika mikopo		**-**	(2,157,841)
Mabadiliko katika madeni ya upangishaji		**25,784**	(8,529)
Gawio lililolipwa	**30**	**(2,630,394)**	(1,910,363)
Jumla ya fedha taslimu zilizotumika katika shughuli za ufadhili		**(2,604,610)**	(4,076,733)
Jumla ya mabadiliko ya fedha taslimu kwa mwaka		**(1,570,563)**	(4,463,719)
Fedha taslimu mwanzoni mwa mwaka		**2,241,156**	6,704,875
Jumla ya fedha taslimu mwishoni mwa mwaka	**15**	**670,593**	2,241,156

WEKEZA

SASA NA


AFRIPRISE
INVESTMENT PLC.



Government Securities | NSE & RSE |
Marketable Securities on DSE | Corporate Bonds
Fixed deposits.

WASILISHO

Ndugu wanahisa mnaombwa kupokea na kuridhia taarifa ya kampuni na taarifa ya fedha iliyokaguliwa kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2025 na kuazimia kama ifuatavyo.



"Azimio la 2/2025

Taarifa ya Mwaka ya Wakurugenzi na Taarifa ya Fedha iliyokaguliwa kwa kipindi cha Mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2025 imepitishwa kama ilivyowa silishwa."

KUTANGAZA GAWIO

KUTANGAZA GAWIO

Kwa mwaka ulioishia Desemba 31/2025, inapendekeza gawio la **shillingi 23** ukilinganisha na gawio la **shillingi 18** kwa mwaka 2024.

WASILISHO

Bodi inapendekeza kuwa kama Mkutano Mkuu utaridhia pendekezo hili, malipo ya gawio kwa wanahisa yafanyike baada ya kupitisha azimio hili. Kwa wanahisa ambao wana akaunti za benki malipo yatalipwa kupitia kwenye akaunti zao na kwa njia ya mitandao ya simu.

> *"Azimio la 3/2025*
>
> *Mkutano Mkuu umeazimia na kuridhia pendekezo hili kwamba gawio la shilingi za Kitanzania ishirini na tatu (23) kwa kila hisa kama ilivyopendekezwa na Bodi ya Wakurugenzi."*



UTEUZI WA MKAGUZI WA MAHESABU YA KAMPUNI KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA DESEMBA 2026

Kama ilivyoelezwa kwenye Taarifa ya Mahesabu ya Kampuni kwa mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2025, mahesabu ya Kampuni yalikaguliwa na Kampuni ya Ukaguzi wa Mahesabu na Ushauri ya **Auditax International.**

WASILISHO

Bodi inapendekeza **Auditax International** iteuliwe tena kuwa Wakaguzi wa Mahesabu ya Kampuni kwa mwaka wa fedha unaoishia **Desemba 31, 2026.** Ada ya ukaguzi inayopendekezwa ni **Shilingi Milioni 22 (22,000,000)** kabla ya kodi.

Ada hii imezingatia mwenendo wa soko kwa taaluma ya uhasibu na ukaguzi, ukuaji wa shughuli za Kampuni, uhitaji wa ukaguzi kwa kampuni iliyoorodheshwa katika soko la hisa, pamoja na mfumuko wa bei nchini.

> *"Azimio la 4/2025*
>
> *Auditax International imeteuliwa rasmi kwa mwaka wa fedha 2026 kwa ada ya TZS 22,000,000/= (kabla ya kodi). Mkataba wa kazi uandaliwe."*



PENDEKEZO KUHUSU MALIPO YA WAKURUGENZI

Malipo ya Wajumbe wa Bodi, [Directors fees] yameainishwa kwenye Katiba ya Kampuni. Kifungu Namba 70 [i] kinaeleza kuwa: "The remuneration of the Directors shall from time to time be determined by the Company in General Meeting".Malipo haya huwa yanawekwa kwenye Bajeti ya Kampuni kila mwaka. Malipo ya Wajumbe yanatokana na ukweli kuwa Wajumbe wa Bodi hutumia muda mwingi kusimamia shughuli za Kampuni, badala ya kusimamia shughuli zao binafsi.

Ikumbukwe kuwa Wajumbe wa Bodi ndio wanawajibika kwa Mkutano Mkuu kwa kusimamia shughuli za Kampuni kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002, pamoja na kanuni na taratibu zilizowekwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) na Soko la Hisa la Dar-es-Salaam, utawala bora na ufanisi wa Kampuni. Kwa kifupi chini ya Sheria ya Makampuni, Wajumbe wanawajibika kuhakikisha kuwa wanasimamia vema Kampuni ili wanahisa wasipoteze fedha zao na kwamba mtaji wa Kampuni unakua.

WASILISHO

Kwa kuzingatia matokeo ya shughuli za Kampuni kwa Mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2025, Menejimenti inapendekeza kuwa Wajumbe wa Bodi walipwe Shilingi milioni sita na laki mbili (Shilingi 6,200,000).

> *"Azimio la 5/2025*
>
> *Imeazimiwa malipo ya wakurugenzi wa Bodi yawe shilingi 6,200,000 kwa kila mjumbe"*



KUFUNGA MKUTANO

MKUU WA ISHIRINI NA MOJA

KUFUNGA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA MOJA



AFRIPRISE
INVESTMENT PLC.

JIHAKIKISHIE KESHO YAKO, LEO

KWA KUWEKEZA

KATIKA AFRIPRISE

-Dhamana za Serikali | NSE na RSE
-Dhamana zinazouzwa katika
Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE)
-Hati Fungani za Makampuni
-Amana za Muda Maalumu.



@Afriprisetz

www.afriprise.co.tz

MKUTANO MKUU 20

WA AFRIPRISE INVESTMENT PLC

KIAMBATANISHO 1 - MAHUDHURIO

JUMLA YA HISA ZILIZOLIPIWA:

SNO	JINA LA MWANAHISA	AINA YA UWAKILISHI	
1	ALEXANDER TONGORI MACHANGO		shareholder
2	BARTHOLOMEW MAJOR KUNZUGALA		shareholder
3	BONIFACE DONALD MAKERE	JOSEPH MATANGA KAHUNGWA	Proxy
4	CHARLES MALABA MBUSHI		shareholder
5	CYPRIAN GEOFREY MWELLAH		shareholder
6	DOMINIC DANIEL KYARUZI		shareholder
7	DORICE ADRIAN MAGAYANE		shareholder
8	DR. DOROTHY MARTIN MASOZA		shareholder
9	DR.TUMAINI EDWARD MHADA	JOSEPH MATANGA KAHUNGWA	Proxy
10	DR.VICENT ISAAC MHADA	JOSEPH MATANGA KAHUNGWA	Proxy
11	EVANS EDDY MLAY		shareholder
12	HILDA KOKULAMUKA TEGAMAISHO	LISIUS LADISLAUS	Proxy
13	JAMES MAJUKANO GEGE	JOSEPH MATANGA KAHUNGWA	Proxy
14	KANYENYE KISULILA MATANGA		shareholder
15	MICHAEL DANIEL KAVUTA		shareholder
16	MOHAMED BURHAN	JOSEPH MATANGA KAHUNGWA	Proxy
17	MWIDINI BAKARI MNALI		shareholder
18	SHABANI RAMADHAN ZAMBO	ADAM SHABAN ZAMBO	Proxy
19	TCCIA MOROGORO		shareholder
20	WINFRIDA ELIAB CHIDUO		shareholder
21	ABBASI EXPORTS LIMITED	BENEDICT MUSHI	Proxy
22	AGAPE AMADEUS KAMAGENGE		shareholder
23	ALEX FELIX MAJOH		shareholder
24	ALOYCE SANULA SWILA		shareholder
25	AZIZI HASSANI HARUNA		shareholder
26	BHAVIT KAMALNAYAN BHATIA		shareholder
27	BRIGHTON MANYAMA AIDAN		shareholder
28	CHRISTOPHER MWITA GACHUMA	JOSEPH MATANGA KAHUNGWA	Proxy
29	CLAUDI COSMAS MFUNGO		shareholder
30	COSMAS ADAM MKONDE		shareholder
31	DAYAN REUBEN OLEKUNEY		shareholder
32	DEOGRATIAS ATHANAS MROSSO		shareholder
33	DOMINIC BEDA MASSAWE		shareholder
34	ELISHA JOSEPH		shareholder
35	EMMANUEL JOHN CHINGO		shareholder

36	ERICK ELIEZER BALIGE		shareholder
37	GASPAR KABACHUBYA MUNYAGI		shareholder
38	GODFREY MEITAMEI MOLLEL	FADHILI GODFREY MOLLEL	Proxy
39	GREGORY JOHN MUSHI		shareholder
40	HABAKUKI HUSSEN MAKAO		shareholder
41	HENRY GEORGE MBOTTO		shareholder
42	HERMAN PATRICK GOODLUCK		shareholder
43	HERY EDSON MWIDUNDA		shareholder
44	IGROWTH MANAGED FUND	FRANCIS SAMKYI	Proxy
45	IPYANA PHILBERT MWANKEMWA		shareholder
46	IRENE BAHOYA KULOLA		shareholder
47	ISARIA KAWEDI MWENDE		shareholder
48	IVO JULIUS MATEE		shareholder
49	JAVAN MUGANDA PERE		shareholder
50	JOAN JAMES MNGODO		shareholder
51	JONATHAN SHAURI KARAZE	JOSEPH MATANGA KAHUNGWA	Proxy
52	JOSEPH MARTINI NDEDELA		shareholder
53	JOYCE MWIYA GACHUMA	JOSEPH MATANGA KAHUNGWA	Proxy
54	KELVIN LUCAS MALLYA		shareholder
55	LAURA SYLVESTER MATTUNDA		shareholder
56	LILIAN KOKUSHERULA NYOMBI		shareholder
57	LYAMBA, JULIUS NG`WANANNOGU		shareholder
58	MAANYA MOHAMED SOLISI		shareholder
59	MARY L MTAVANGU		shareholder
60	MASAIDA MUSSA CHIWINGA		shareholder
61	MASIMBA CLEMENT KAKA		shareholder
62	MNANKA GEBANI WINANI		shareholder
63	MWANZA COMMUNITY INVESTMENT PLC	JOSEPH MATANGA KAHUNGWA	Proxy
64	NATHAN EDWARD MNYAWAMI		shareholder
65	OGARA GABRIEL SASSI		shareholder
66	OMARY RUFUNGURO KUPERELWA		shareholder
67	PASCHAL PHINEHAS SARUNGI		shareholder
68	PASTOR PETRI MFOY	TIB RASILIMALI LTD	Proxy
69	PETER WILLIAM KIFUNGUOMALI		shareholder
70	PUBLIC SERVICE SOCIAL SECURITY FUND	HERMAN GOODLUCK	Proxy
71	RAMADHANI ZAIDI RUPIAH		shareholder
72	SARA DONALD MREMA		shareholder
73	SIMON JOHN KESSY		shareholder
74	STELLA MARO HIRJI		shareholder
75	STEVEN EMANUEL GOSSI		shareholder
76	SYNPHOROSE EVARIST BAITWA		shareholder
77	THERESIA SAMSON MUSHI		shareholder
78	VINCENT BERNARD MSAKI		shareholder

79	WAHAB HASHIMU SHOO		shareholder
80	WARIALANGA AMOS MBISE		shareholder
81	YAKOBO MARUKUSI MAHAY		shareholder
82	ZUM SERVICES LIMITED		shareholder

LAYOUT & DESIGN:
INFINITY BRANDS (T) LTD
Mob: +255 624 400 295 | 717 200 295
E-mail: mudithan@mail.com

AFRIPRISE INVESTMENTS PLC
PSSSF Millenium Tower II, 24th Floor
P. O. Box 72678, Dar es Salaam, Tanzania
Mobile: +255 753 701 802 | **Email:** info@afriprise.co.tz
www.afriprise.co.tz